HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA
TOLEO LA 001 | MACHI 2024 | HALIUZWI

# CHUNYA

Jarida la Mtandaoni

## ZAWADI YETU



MHARIRI MKUU
TAMIM H. KAMBONA
Mkurugenzi Mtendaji wilaya ya Chunya

MHARIRI MSAIDIZI
JOSHUA. A. SENGO
Kaimu Mkuu wa kitengo cha Habari Wilaya ya Chunya
FATUMA MTWEVE
Afisa Habari-Wilaya ya Chunya

WAPIGA PICHA
JOSHUA A. SENGO
FATUMA MTWEVE
FRANK T. LYIMO

MSANIFU WA JARIDA
FRANK T. LYIMO
Afisa Habari-Wilaya ya Chunya

# UONGOZI WA WILAYA YA CHUNYA




Mhe. Mbarak Alhaji Batenga
Mkuu wa wilaya ya Chunya



Mhe. Bosco Mwanginde
Mwenyekiti H/Shauri ya Chunya



Mhe. Masache Njelu Kasaka
Mbunge Jimbo la Lupa



Ndugu; Anakleth Michombero
Katibu tawala wilaya ya Chunya



Ndugu; Tamim Kambona
Mkurugenzi Mtendaji - Chunya

# MARUFUKU UCHIMBAJI WA MADINI NDANI YA MTO ZIRA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mhe. Suleiman Jafo, ameuongozi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya, na Taasisi nyingine zinazohusika kuhakikisha hakuna mto yeyote, mwekezaji na mtu mwingine yeyote asiruhusiwe kufanya Uchimbaji wa madini ndani ya Mto Zira mpaka pale wataalamu watakapo jiridhisha juu ya Utunzaji wa Mazingira kwa mujibu wa sharia zinazoongoza uchimbaji wa madini.

Mhe. Jafo alitoa kauli hiyo mapema Januari 19, 2024 baada ya kufanya ziara ya kutembelea na kukagua kampuni ya G&I inayofanya shughuli za Ujichambaji wa madini katika Mto Zira wilayani Chunya.

"Hawa wawekezaji wote hakuna mtu atakaye ruhusiwa kufanya uchimbaji humu lazima kwanza wataalamu wangu wa Mazingira wajiridhishe kwamba hilo jambo linawekezekana na linawezekana vipi na kuhakikisha mazingira yanalindwa".

Aidha Mhe Jafo aliagiza pia wawekezaji wote kwenye ukanda wa Mto Zira wanaofanya shughuli zao za uchimbaji wa madini ya Dhahabu kuhakikisha wana kamilisha tathimini ya uaribifu wa Mazingira na ndipo taratibu zingine ziendelee na aliwataka Wataalamu toka ofisi yake kuhakikisha hiyo tathimini ya mazingira iwe na masharti mahususi yatakayo ainisha mambo yanayotakiwa kufanyika na wahusika.

Wakati akitoa salamu za wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa Mhe Waziri, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Zuberi Homera alisema ana amini kwenye teknolojia kwani wakiwekeza kwenye teknolojia wanaweza kuchimba dhahabu na maji yasichafuke na hata mazingira yasiaharibiwa kabisa.

"Tukienda kwenye Nchi za wenzetu huko wanateknolojia nyingi sana maji yanaweza yasichafuke na watu dhahabu wakaondoka nayo, kitu kikubwa ninacho sisitiza hapa huyu mwekezaji awekeze kwenye teknolojia ili madini yaweze kutoka kwa masilahi mapana ya Nchi yetu" alisema Mhe. Homera

Mhe Homera aliongeza kusema uwezo wa kuwekeza kwenye teknolojia ni mkubwa huku akisema kama imewezekana kuchimba visima vya maji katika kata mbalimbali za Halmashauri ya wilaya ya Chunya watu wanapata maji safi na salama bila shaka hivyo hata kuwekeza kwenye teknolojia haiwezi kushindikana hatimaye dhahabu ichimbwe bila kusababisha madhara yoyote.

Katika ziara hiyo Mhe Jafo alitembelea kiwanda cha kuchenjua Dhahabu cha Anglo De Beers kilichopo kitongoji cha Mwaoga kata ya Makongolosi Mamlaka ya Mji mdogo Makongolosi wilayani Chunya ambapo aliwapongeza wawekezaji wa kiwanda hicho kwa uwekezaji mkubwa na kutengeneza ajira kwa watanzania wakiwepo wananchi wa wilaya ya Chunya.

# TENGENI MAENEO YA KUJENGA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA VIJIJI NA KATA



Kamati ya fedha, Uchumi na Mipango ya Halmashauri ya wilaya ya Chunya imeagiza viongzoi wa vijiji na kata zote za Halmashauri ya wilaya ya Chunya kutenga maeneo ya kujenga miundombinu ya maendeleo katika vijiji na kata zao ili kuepuka kutumia fedha za mradi kulipa fidia watu wenye maeneo pindi mradi utakapoanza kujengwa

Maagizo hayo yalitolewa tarehe 11/1/2024 wakati kamati hiyo ilipotembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari ya kata ya Kambikatoto ambayo tayari imeshaanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2024 huku wanafunzi 88 wamepangwa kuripoti katika shule hiyo kwa mwaka wa masomo 2024

Akitoa maoni wakati wa ziara hiyo makamu mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya Mhe Ramadhani Shumbi kwaniaba ya kamati hiyo alisema haiwezekani kutumia fedha zilizotengwa kwaajili ya mradi Fulani kulipa fidia watu wenye maeneo wakati Serikali ina maeneo makubwa kuliko wananchi wa kawaida.

“Haiwezekani milioni tatu na laki tatu kutumika kuwalipa fidia wananchi ili kupisha eneo la kujenga shule maeneo ya vijijini

kama Kambikatoto kwani fedha hizo zingetumika kwaajili ya kuendeleza miundombinu mingine ambayo ni muhimu, Sasa ni lazima viongozi wa vijiji na



kata kutenga  maeneo yatakayotumika kujenga miradi ya maendeleo hii ya kulipa fidia haitakiwi kuwepo kwa maeneo kama haya ya wilaya yetu" Alisema Mhe Shumbi.

Mhe Sailon Mbalawata diwani wa kata ya Bwawani na mjumbe wa kamati hiyo ameshauri viongozi wa kata kuhakikisha eneo la shule lenye ukubwa wa hekari 21.5 linahifadhi vizuri kwa kuhakikisha hati zake zinapatika kwa wakati kwani kuchelewa kufanya hivyo inaweza kuleta usumbufu usio wa lazima hapo baadaye.

Aidha wajumbe wa kamati wameshauri viongozi wa kata hiyo kuongeza juhdi kuhakikisha wanafunzi wote waliopangwa kuripoti  shule hiyo kwa mwaka wa masomo 2024 wanaripoti haraka iwezekanavyo hadi kufikia tarehe 25/1/2024 wanafunzi wote wawe wemeripoti tayari kuanza muhula wa masomo kama serikali inavyotaka, Mpaka machi 21, 2024 zaidi ya asilimia 80 ya wanafunzi waliopangwa kuripoti shule ya sekondari Kambikatoto wameripoti na wanaendelea na masomo

Katika siku ya kwanza ya ziara ya Kamati ya Fedha, uchumi na Mipango yenye thamani ya shilingi milioni 697,180,000/= ambayo ni pamoja na Mradi wa ujenzi wa Shule ya sekondari kambikatoto iliyopewa shilingi milioni mia tano na themanini na tatu (583, 180,000/=), mradi wa ukamilishaji wa madarasa mawili na  matundu sita ya vyoo shule ya sekondari Bitimanyanga ambayo ilipewa shilingi milioni thelasini na moja (31,000,000/=) pamoja na mradi wa Ujenzi wa Shule shikizi ya msingi Tulieni iliyopewa shilingi milioni themanini na tatu (83,000,000/=)

# MAEENEO YOTE YA SERIKALI NA TAASISI YAPIMWE ILI KUEPUSHA UVAMIZI

Mkuu wa wilaya y Chunya Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiaji  Mhe Mbarak Alhaji Batenga ameagiza maeneo yote ya Serikali pamoja na Taasisi zote kupimwa kwa haraka sana na kupatiwa hati ili kuepuka uvamizi na migogoro inayojitokeza kati ya wananchi na serikali au serikali na wananchi jambo linalothili ushirikiano kati ya serikali na wananchi wake

Mhe Batenga alitoa kauli hiyo tarehe 15/01/2024 wakati akihutubia mkutano wa handara kwenye viwanja vya ofisi ya serikali ya kitongozji cha Itumbi baada ya kuhitimisha ukaguzi wa barabara za Mnazi Mmmoja-Sambilimwaya yenye urefu wa kilometa tatu (3) na Barabara ya Matundasi-Itumbi yenye urefu wa kilometa kumi na mbili (12).

Ziara hiyo ilihusisha kamati ya Usalama ya wilaya ya Chunya pamoja na Meneja wa Meneja wa wakala wa barabara za vijijini na mijini (TARURA) mkoa wa Mbeya

"Wiki ijayo mpima ardhi afike hapa, katibu tawala simamia hilo ili maeneo yote ya Serikali hapa Itumbi na Maneneo mengine ya wilaya yetu yapimwe na yapewe hati ili tuone uvamizi unatokea wapi na hii ndo itakuwa suluhisho la migogoro ya ardhi ndani ya wilaya ya Chunya na vijiji vyake"

Aidha Mkuu wa wilaya ya Chunya amewataka wananchi wa wilaya ya Chunya kuendelea kuiamini Serikali ya awamu ya sita chini Rais Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwani ni sikivu na inawapenda wananchi wake na inatatua changamoto mbalimbali



zinazowakabili wananchi wake kwa wakati ili kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali ili wananchi wake waendelee na shughuli za uzalishaji mali.

Migogoro ya Ardhi imekuwa ikijitokeza katika maeneo mbalimbali ya Nchi yetu ikiwa ni pamoja na wilaya ya Chunya hivyo viongozi wa serikali kwakushirikiana na wananchi wa maeneo husika ni jukumu lao kuhakikisha migogoro hiyo inatatuliwa na pia kushirikiana kuzuia migogoro mingine isijitokeza, Jambo hilo linawezekana kama kila mmjoa akitambua umuhimu wa kushirikisha serikali katika umilikishaji wa ardhi.

Wakati wa Mkutano huo wa Hadhara na Mkuu wa wilaya baadhi ya wananchi akiwepo Oden Mwakanyamale alieleza eneo la Makaburi kuuzwa na hakuna eneo lingine lililotengwa kwaajili ya Makaburi, Twalibu Athuman yeye pia alieleza namna anavyosumbuliwa juu ya umiliki wa shamba lake wakati alinunua kihalali na mtu aliyemuuzia yupo na ushahidi upo

Ziara ya Mkuu wa wilaya kutembelea maeneo mbalimbali ya wilaya ilikuwa ni kutekeleza maelekezo na ushauri uliotolewa na kamati ya siasa ya Chama cha Mapinduzi wilaya ya Chunya ilipofanya ziara yake ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambapo changamoto mbalimbali zilibainishwa na kamati hiyo ikiwepo migogoro ya ardhi.

# TARURA WASHAURIWA KUPELEKA BAJETI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWENYE BARAZA LA MADIWANI



Kamati ya fedha Uongozi na Mipango ya Halmashauri ya wilaya ya Chunya kwa niaba ya Baraza la Madiwani imewataka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wilaya ya Chunya kupeleka bajeti zao pamoja na mapendekezo ya miradi wanayoitekeleza kwenye kamati hiyo ili kuamua kwa pamoja mradi upi uanze kuteklezwa na kwa gharama ipi mradi husika utatekelezwa kwani Madiwani ndio wanaoishi na wananchi hivyo wana uelewa mkubwa juu ya mahitaji ya wananchi wanaowaongoza.
Maoni hayo yametolewa na wajumbe wa kamati ya fedha, uchumi na mipango ya Halmashauri ya wilaya ya Chunya wakati wa ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwepo daraja la Lualaje linalogharimu shilingi milioni mia mbili na kumi (210,116,000/=), Ujenzi wa daraja la Magunga kupitia barabara ya Ngwala linalojengwa kwa shilingi 178,214,000/= pamoja na mradi wa ujenzi wa Barabara ya Malangamilo yenye urefu wa kilomita 8 yenye thamani ya shilingi milioni 274,885,000/=
“Sasa tunaandaa bajeti ya mwaka 2024/2025 na nyinyi TARURA muwe mnatuletea bajeti yenu kwenye vikao vya kamati ya fedha ili na sisi tupate nafasi ya kushauri barabara ipi ipewe kipaumbele Zaidi lakini pia kuhakikisha bajeti inayopangwa inaenda sambamba na uhalisia tunapoenda kukagua miradi” Alisema Mhe Mwanginde
Aidha kamati hiyo imeagiza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wilaya ya Chunya kuhakikisha wanafuatilia agizo la Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha barabara zinazoenda kwenye maeneo ambayo miradi ya Build Better Tomorrow (BBT) itatekelezwa zinafunguliwa



ili kurahisisha utekelezaji wa mradi ili lengo la Serikali la kuanzisha mradi huo litimie kama ilivyo kusudiwa “Leo ni tarehe 12/1/2024 naomba kufikia tarehe 20/1/2024 mlete taarifa in-



ayoonesha tayari bajeti ya kufungua barabara hizo ime-tengwa ili kamati hii ipate namna ya kuendelea kufuatil-ia utekelezaji wa suala hilo kama Mhe Rais alivyoagiza” Aliongeza Mhe Mwanginde

Akizungumza na kujibu hoja za wajumbe wa kamati hiyo Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wilayani Chunya Mhandisi Emannuel S Kayola amesema miradi yote in-aendelea vizuri lakini maoni, mapendekezo na Maelekezo ya wajumbe wameyachukua na watayafanyia kazi ili kuwa na uelewa wa pamoja wakati wa ukaguzi na usimamizi wa miradi husika.

Ziara ya Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Hal-mashauri ya wilaya ya Chunya ilikuwa ziara ya kawaida ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa wilayani Chunya, Katika ziara hiyo kamati ilikagua mira-di yenye thamani ya shilingi milioni 663,215,000/= ambayo inasimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wilayani Chunya.



Mhe. Bosco Mwanginde
Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya

# DC BATENGA: "SHULE ZOTE CHUNYA ZIWE NA MASHAMBA YASIYOPUNGUA HEKARI 10"

Mkuu wa Wilaya ya Chunya Mhe Mbarak Alhaji Batenga ameagiza Shule zote wilayani Chunya kuwa na Mashamba yasiyopungua hekari kumi ili mazao yatakayopatikana yatumike kama chakula kwa wanafunzi jambo ambalo litawaondolea wazazi na walezi mzigo wa kuchangia huku akiagiza Maafisa Ugani kusimamia Mashamba hayo vizuri ili kuwawezesha wananchi wengine kuja kujifunza mbinu mbalimbali za kilimo chenye manufaa.



Maagizo hayo aliyatoa wakati aliposhiriki kikao cha kamati ya Lishe cha Robo ya pili ya mwaka 2023/2024 kilichoketi katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya wilaya uliopo jengo jipya la utawala chenye lengo la kutathimini mwenendo wa hali ya Lishe katika wilaya ya Chunya na kuchukua hatua stahiki kuhakikisha mikata ya Lishe inatekelezwa ipasavyo katika Halmashauri ya wilaya ya Chunya.

"Tunakwenda kutengeneza mashamba darasa katika shule zetu zote wilayani Chunya. Shule ziwe na Mashamba yasiyopungua heka kumi (10) na mazao yanayopatikana yatumike kwaajili ya chakula shuleni na maafisa ugani wa kata wasimamie mashamba hayo, Kwakufanya hivyo lile lengo la kushika nafasi ya kwanza kitaifa katika utekelezaji wa mkata wa Lishe litafanikiwa" Alisema Mhe Batenga.

Katika nafasi nyingine Mhe Batenga alimpongeza Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ndugu Tamim H Kambona kwa juhudi kubwa alizofanya na anzoendelea kufanya katika kusimamia utekelezaji wa mkataba wa lishe ambapo kupitia juhudi hizo wilaya ya Chunya kwa mara tatu mfululizo imeshika nafasi ya tatu kitaifa katika utekelezaji wa mkataba wa Lishe na sasa Chunya inataraji kushika nafasi ya kwanza kitaifa katika utekelezaji wa Mkataba wa Lishe.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya Ndugu Tamim Kambona amewataka Idara tumizi na simamizi ya Lishe kuhakikisha fedha zote zilizotengwa kwaajili ya utekelezaji wa afua za lishe zinatumika kama ilivyokusudiwa kwani yeye katika ofisi yake ni kuhakikisha fedha zinapatikana lakini kazi ya kusimamia iko chini ya Idara zinazohusika kutumia na kusimamia fedha hizo.

"Hatutaki taarifa za mwisho zinakuja zinaeleza eneo Fulani tuna asilimia 99.9 au asilimia chini ya hapo, sisi tunachotaka kila eneo tunafikia asilimia 100 na kama tunaruhusiwa hata Zaidi lakini sitaki kuona tuko chini ya asilimia 100 eneo lolote la utekelezaji wa mkataba wa Lishe, naomba idara simamieni hili"

James Sunge kaimu Mkuu wa idara ya Maendeleo ya jamii, Mw Abdalah Mchelu kaimu mkuu wa idara ya elimu ya Awali na Msingi, Mw Konzeta Ngachenga kaimu mkuu wa idara ya elimu Sekondari na Nicholaus Chambala kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo na Mifugo walihudhuria kikao hicho na waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa afua za lishe kwa kipindi cha robo ya pili pamoja na mikakati ya Idara wanazoziongoza kuhakikisha kile kilichokusudiwa kinafikiwa kwa wakati na kwa weledi

Kikao cha kawaida cha kamati ya lishe wilaya ya Chunya kimeketi leo tarehe 16/2/2024 kikiwa na lengo la kufanya tathimini ya utekelezaji wa Mkataba wa lishe kwa Robo ya pili jambo ambalo hutoa dira juu ya kinachoendelea kufanyika katika kipindi cha Robo ya tatu ikiwa ni pamoja na kurekebisha panapoonekana kukwamisha utekelezaji wa Mkataba wa Lishe.




# FAIDA MNAYOPATA LAZIMA IONEKANE KWENU NA KWA JAMII YENU

Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Halmashauri ya wilaya ya Chunya imewataka wanawake, vijana na wale wenye ulemavu wanaonufaika na mkopo wa asilimia 10 ambazo ni fedha za serikali zinazotokana na mapato ya Ndani kuhakikisha matunda ya kukopeshwa kwao yanaonekana kwa walengwa kwanza na baadaye kwa jamii inayowazunguka kwakufanya hivyo watakuwa wametimiza lengo la serikali la kuwainua wananchi wake kiuchumi.

Baraza la Madiwani kupitia kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango walitoa ushauri huo wakati kamati hiyo ilipotembelea kikundi cha Wanawake Jamii kilichopo kata ya Lupa ili kujionea shughuli zinazofanywa na kikundi hicho tangu kilipoanza kukopeshwa na Halmashauri ya wilaya ya Chunya mwaka 2019 kwa fedha zinazotengwa kwaajili ya kuwakopesha vijana wanawake na wenye ulemavu maarufu kama asilimia kumi.

"Kile mnachokipata kama faida lazima tukione kwenu kama wanakikundi na baadaye tukione kwa jamii inayowazunguka, nje ya hapo maana yake lengo la ninyi wanawake, vijana na wenye ulemavu la kukopeshwa na Serikali inayoongozwa na Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan litakuwa bado halijatimia hivyo lazima tuone mabadiliko kwanza kwenu ninyi wenyewe na baadaye jamii yenu" Alisema Mhe Shumbi.

Kamati hiyo pia imewapongeza wanawake wa kikundi hicho kwakurejesha fedha walizokopeshwa lakini pia kwa namna ambavyo hawakukata tamaa baada ya mradi wao wa kufuga kuku kushindwa kuendelea kutokana na changamoto mbalimbali na kuamua kuhamia kwenye mradi wa kufuga Nyuki huku lengo lao likibaki kuwa la kujikwamua kiuchumi.

Kamati hiyo imewashauri kikundi cha wanawake Jamii

kuona uwezekano wa kumiliki misitu yao wenyewe ili kurahisisha utekelezaji wa mradi wao wa ufugaji wa Nyuki jambo litakalo wasaidia kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu kwenye misitu mbalimbali ambayo hutumika kama maeneo yao ya kuweka mizinga.
Wakati akitoa taarifa ya mradi wa kikundi hicho Mwenyekiti




wa kikundi hicho Bi Vumilia Kilindu amesema faida wanazopata wanakumbuka kurudisha kwa jamii inayowazunguka kwani mpaka sasa wamechangia mifuko kumi ya saruji katika ujenzi wa shule ya Msingi Lupatingatinga, wametoa msaada wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya laki tano (500,000) kwa wanafunzi wasiojiweza kwenye shule ya msingi Lupatingatinga na wataendeleo kufanya hivyo kadiri wanavyoendelea kupata faida.
Akitoa salamu za Shukrani kwa kamati hiyo Mhasibu wa kikundi hicho Bi Delista Hyera ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia uongozi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya kwanza kuwakopesha fedha na kuendelea kuwapa ushauri wa mara kwa mara, pamoja na kutembelewa na maafisa maendeleo ya Jamii lakini amesema ushauri na maelekezo ya kamati hiyo wameupokea kwa dhati na wataufanyia kazi ili waendelee kufanya vizuri zaidi
Kikundi hicho mpaka sasa kina jumla ya wanachama 16, kikundi hicho kinamiliki mzinga zaidi ya mia mbili ambapo 151 tayari imewekwa katika msitu mbalimbali na 57 iko tayari muda si mrefu itapelekwa kwenye msitu wa Inyonga ulioko kata ya Mafyeko na huwa wavuna karibu lita mia tano za asali na kuziuza hatimaye kuboresha maisha yao kama wanakikundi na baadaye  kurudisha kwa jamii inayowazunguka

# MKAITUMIE ELIMU YA ARDHI MNAYOIPATA KUWAELIMISHA WANANCHI

Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya Mhe. Bosco Said Mwanginde amewataka wadau wa masuala ya ardhi kuhakikisha elimu wanayokuwa wameipata katika Mafunzo mbalimbali wanayoyapata wanaitumia katika kuelimisha wananchi wengine kuhusu ardhi katika maeneo wanayotoka ili kuziua migogoro inayojitokeza kutokana na kukosa uelewa wa Masuala ya sharia ya ardhi Kauli hiyo aliitoa Februari 28, 2024 wakati akifungua kikao cha wadau wa ardhi katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya uliopo jengo jipya la utawala, kilicho andaliwa na taasisi ya MIICO inayotekeleza mradi wa Uendelezaji na upatikanaji wa ardhi bora kwa wazalishaji wadogo Nyanda za juu kusini mwa Tanzania ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Chunya katika kata ya Sangambi na Upendo kilichoketi

"Kaitumieni elimu mnayoipata huko mnakokwenda na kwenye majukwaa yenu wajue nini mnakifanya,- madiwani mliopo hapa kule mnakotoka huwa kunakuwa na migogoro ya masuala ya ardhi, mkajitahidi kuelimisha lakini pia watendaji wa kata na ninyi pia mkasimamie haya mtakayoyapata katika mafunzo haya huko kwenye maeneo yenu"alisema Mhe Mwanginde.




Afisa mradi kutoka MIICO Bi Glory Mdindile akieleza malengo ya Mkutano pamoja na mpango kazi wa taasisi

hiyo alisema lengo kuu ni kutambulisha mradi katika awamu ya nne ya utekelezaji lakini pia kushirikishana mipango kazi na wadau wengine kwenye masuala ya ardhi ikiwa ni pamoja na kujua shughuli mbalimbali zinazofanywa na wadau katika masuala ya ardhi.
Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ndugu Athuman Bamba ambaye ni mwanasheria wa Wilaya ameishukuru taasisi ya MIICO kwa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya masuala ya ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya na kutoa rai kwa watendaji na wenyeviti wa vijiji wa maeneo husika kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa taasisi hiyo.
Afisa kilimo na Mifugo wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya ndugu Cuthbert Mwinuka alieleza mipango mikakati iliyowekwa na Divisheni ya Kilimo na mifugo Halmashauri ya wilaya ya Chunya katika kupambana na changamoto za migogogro ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuanzisha mashamba ya lanchi kwaajili ya wafugaji lakini pia kuendelea kuwaelimisha wananchi kila mmoja kuheshimu mipaka yake kulingana na jinsi maeneo yalivyotengwa kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi
Faraja Kyando mwakilishi wa wakulima Sangambi, Reonald Manyesha Mwenyekiti wa wachimba madini Mkoa wa kimadini Mbeya na Shangai Rapoy mwenyekiti wa Chama cha wafugaji Wilaya ya Chunya ni miongoni wa wadau waliowasilisha changamoto wanazo kabiliananazo katika masuala ya ardhi kubwa ikiwa ni migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima pamoja na wachimbaji wa madini katika maeneo yao
Kikao hicho kilihusisha wadau mbalimbali wakiwemo waheshimiwa madiwani wa maeneo unakotekelezwa mradi ,wadau kutoka Azaki mbalimbali, Wakulima, Wafugaji, Wachimbaji wa Madini, Wakuu wa idara, watendaji wa kata na Wenyeviti wa vijiji. Kikao hicho kilazimia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwaomba watu wa madini wasitoe lesseni mpaka wafike eneo husika na kujiridhisha kama halina Migogoro yoyote.



# FYANDOMO "WANAWAKE TUNAAMINI HATUSHINDWI"




Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya Mhe.Suma Fyandomo amewataka wanawake kujitokeza kuchukua fomu na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwani uwezo wanao na hawashindwi kutekeleza majukumu mbalimbali ya Kifamilia, Kijamii na kitaifa kwa ujumla huku akisistiza kuondoa hofu wakati wa kufanya jambo lolote

Kauli hiyo ameitoa leo tarehe 05 Machi 2024 wakati wa maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani kiwilaya yaliyofanyika katika viwanja vya Msifuni kijiji cha Ifuma kata ya Lupa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ikiwa ni kuadhimisha siku ya wanawake kiwilaya .

"Wanawake niwatie moyo kwenye nafasi zozote zinapojitokeza msisite, msiogope mnatakiwa kusonga mbele kuwa mstari wa kwanza kwenda kuchukua fomu au kuomba nafasi hizo kwasababu wanawake tunaamini hatushindwi , wanawake ni Jeshi kubwa lakini pia ni nguzo kubwa ya familia"amesema Mhe. Fyandomo.

Aidha Fyandomo ameongeza kuwa wanawake kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza mbele yao akisema ujasiri ndio iwe nguvu ya kuchangamkia fursa hizo kwani uwezo wanao na wanaweza hata wasipowezeshwa huku akirejerea uwezo wa wanawake kukabili majukumu ya Familia zao pindi wakinababa wa familia wanapokuwa

wametelekeza familia zao "Nitumie jukwaa hili kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hasaan kwa kuuvaa Ujasiri wa hali ya juu kuongoza Royal tour ambayo imezaa matunda, watalii wameongezeka lakini pia imetuingizia fedha za kigeni ambazo zimesadia katika kukuza uchumi wetu"alisema Fyandomo.

Akisoma risala kwa Mgeni rasmi katibu wa kamati ya maandalizi ya siku ya Wanawake duniani wilaya ya Chunya Bi Bahati Mwampetele amesema kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imefanya jitihada mbalimbali katika kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuwawekea mazingira wezeshi ya biashara ,kwendelea kutoa elimu kwa jamii kupinga vitendo vya ukatili , kutoa elimu ya malezi na makuzi ili kuwajengea wanawake uwezo wa kujiamini.

Maadhimisho ya Siku ya wanawake duniani huadhimishwa kila mwaka tarehe 8 Machi ambapo kwa Wilaya ya Chunya Maadhimisho hayo yamefanyika leo tarehe 05 Machi 2024, yakienda sambamba na ugawaji wa vifaa mbalimbali kama vile viti mwendo kwa watoto wenye ulemavu, vifaa vya usafi kituo cha Afya cha Lupatingatinga, fedha pamoja na vitu vingine kwa wahitaji






*Mbunge viti Maalum Mkoa wa Mbeya Mhe. Suma Fyandomo alieshika maiki akiwa pamoja na Mbunge wa Jimbo la Lupa Mhe Masache Kasaka akizungumza neno baada ya kukabidhi viti mwendo kwa watoto wenye ulemavu wakati wa maadhimisho ya sikuya wanawake duniani yaliyoadhimisha kiwilaya katika kata ya Lupa kijiji cha Ifuma.*

# JIOGRAFIA YA CHUNYA HAITUZUII KUFANYA VIZURI



Halmashauri ya wilaya ya Chunya iko umbali wa Kilometa 70 kutoka Makao makuu ya mkoa wa Mbeya, ina ukubwa wa kilometa za Mraba 13,149 elfu. Wilaya ya Chunya ina wakazi 344,442 kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022. Jiografia ya wilaya ya Chunya inaweza kuwa jiografia Ngumu kuliko jiografia ya wilaya yoyote ya Mkoa wa Mbeya.

Ni jambo la kawaida kwa maafisa na watumishi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya kusafiri umbali wa Kilometa mia moja kutoka makao makuu ya wilaya kwenda kuwahudumia wananchi, lakini pia kuna maeneo ya umbali wa Zaidi ya kilometa 300 wananchi huishi na hivyo hulazimu maafisa kufika katika maeneo hayo kwaajili ya kupeleka huduma mbalimbali.

Ugumu huo wa kijiografia hauzuii Chunya kufanya vizuri katika maeneo mbalimbali ili kumrahisishia mwananchi wa kawaida kupata huduma kwa wakati. Halmashauri ya wilaya ya Chunya imetoa chanjo ya Surua Rubella kwa watoto 44,942 sawa na asilimia 116.37 wakati lengo lilikuwa kuwafikia watoto 38,619 na kwa takwimu hiyo Halmashauri ya wilaya ya Chunya ilikuwa Halmashauri iliyochanja watoto wengi kuliko wilaya nyingine yoyote ya Mkoa wa Mbeya ukilinganisha na malengo yaliyokuwa yamewekwa awali

Halmashauri imefanya vizuri miaka mitatu mfululizo katika utekelezaji wa afua za lishe ambapo Kitafa Halmashauri ya Chunya ilishika nafasi ya Tatu kati ya Halmashauri 185 zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kwa dhana hiyo katika Mkoa wa Mbeya Halmashauri ya wilaya ya Chunya ilikuwa ya kwanza kwa miaka mitatu mfululizo katika kutekeleza Mkataba wa lishe, Hili sio jambo dogo na la kubezwa

Pia Halmashauri ya wilaya ya Chunya imekuwa ni kawaida kwao kushika nafasi ya kwanza katika ukusanyaji wa Mapato Mbele ya Halmashauri zote saba zinazouunga Mkoa wa Mbeya. Kwakuwa takwimu hizi hutolewa kwa kila baada ya miezi mitatu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ni kwa vipindi vyote vya mwaka 2023 na sasa 2024 Halmashauri imeendelea kufanya vizuri ikizishinda Halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya. Kupitia ukusanyaji mzuri wa Mapato, Halmashauri ya

wilaya ya Chunya imekuwa Halmashauri pekee kuanza kujenga uwanja mkubwa wa Michezo ambao ndani yake kutakuwa na viwanja mbalimbali vya michezo, Na tayari kuna uthibitisho wa wazi kabisa mwaka jana 2023 Mashindano ya SAMIA MBEYA SUPER CUP yaliyohusisha timu kutoka Halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya yalichezwa katika uwanja huo hili pia sio Jambo dogo.



Haya yote yanawezekana kutokana na ushirikiano mzuri uliopo katika ya Ofisi yangu, Ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Chunya, Waheshimiwa Madiwani pamoja na ofisi ya Mhe Mbunge wa Jimbo la Lupa sisi sote kazi yetu ni moja tu ya kuwahudumia wananchi wa wilaya ya Chunya, tukimsaidia Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan na bila shaka jukumu hilo tunalitekeleza vema kama takwimu nilizozitoa hapo juu zinavyoeleza

Lakini pia, niwapongeze wakuu wa idara na vitengo kwa namna wanavyopambana kuhakikisha kazi inaenda vizuri katika maeneo wanayosimamia, maana wao ndio washauri wangu katika maeneo wanayoyasimamia, Matokeo tunayoyapata katika maeneo mbalimbali yanachagizwa na usimamizi mzuri wa wakuu wa idara na vitengo.

Mwisho sio kwa umuhimu, Niwashukuru watumishi wote wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya kwa namna wanavyofanya kazi kwa bidii, kujituma bila kujali changamoto ya mazingira, pengine hata miundombinu ya usafiri kwa maana ya barabara za kutoka eneo moja kwenda eneo lingine ili kuwahudumia wananchi wa wilaya ya Chunya, Naomba niwambie kazi yao, bidii yao ndiyo inayotufanya Chunya kung'ara kimkoa na hata kitaifa.

Niwaombe wananchi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya waendelee kuiamini Serikali ya awamu ya sita Chini ya Jemedari Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya uungano wa Tanzania kwani haya yote yanayofanywa na sisi wasaidizi wake ni maelekezo yake, na pia niwahakikishie tutaendelea kujenga miundombinu mbalibali katika maeneo yenu kwa kushirikiana nanyi

Ahsanteni sana

TAMIM H KAMBONA,
MHARIRI MKUU WA JARIDA

## KUPITIA MAPATAO YA NDANI MIRADI YA KIMKAKATI IMEJENGWA CHUNYA

Halmashauri ya wilaya ya Chunya imejenga miradi yenye thamani ya Shilingi Bilioni 1,715,836,159/= kwa fedha za Mapato ya Ndani baada ya kusimamia vema ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ya wilaya ya Chunya kiasi cha Serikali kuruhusu sehemu ya pamoja na Shule ya Mchepuo wa Kiingeleza ambayo imejengwa katika kata ya Itewe na imegharimu shilingi milioni 448,675,359/= ambapo vyumba saba vinatumiwa na wanafunzi 262 na tayari ujenzi wa madarasa sita unaendelea na upo katika hatua mbalimbali za ujenzi kumesaidia wananchi wengi kupeleka watoto wao katika shule hiyo kwa gharama nafuu ukilinganisha na shule za mtu Binafsi

Kwa sasa Halmashauri inajenga Madarasa manne ambapo shilingi milioni mia moja zimepelekwa ili kuendelaza ujenzi mada-



Makusanyo hayo kutumika kujenga miundombinu ili kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii kwa wananchi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya.

Miundombinu iliyojengwa ni

Kabla ya kujengwa kwa Shule hiyo Halmashauri ya wilaya ya Chunya ilikuwa haina shule ya mchepua wa kiingereza jambo ambalo lilikuwa linawakosesha fursa watoto wenye wazazi ambao wana kipato cha chini. Hivyo kujengwa kwa Shule hiyo

rasa kwaajili ya kuendelea kupokea wanafunzi wengi Zaidi kama ilivyo adhima ya Serikali ya awamu ya sita ya kuwapatia huduma wananchi wake kwa urahisi na ukaribu Zaidi

Ujenzi wa Soko la Madini nao nimradi mwingine ambao umejengwa kwa fedha za Mapato ya ndani huku lengo la mradi huu ni kumsaidia mwananchi wa kawaida



hasa mchimbaji mdogo na mkubwa kuuza madini yake kwenye soko halisi ambapo bei ya dhahabu hujulikana hadharani tofauti na ilivyokuwa mwanzo.

Ujenzi wa Soko la Dhahabu umegharimu Zaidi ya shilingi milioni mia saba (700), ambapo kupitia soko hilo takwimu sahihi ya mauzo ya dhahabu sasa zinafahamika ambapo kwa mwezi inakadiriwa karibu kilogramu 300 mpaka 350 huuzwa katika soko hilo na huingiza karibu milioni 300 kama tozo ya huduma lakini pia kupitia soko hilo Halmashauri inakusanya ushuru wa kupangishi vyumba kwa wafanya biashara, Hivyo vyanzo vya mapato vimeongezeka kwa Halmashauri ya wilaya ya Chunya

Ujenzi wa uwanja unaojumuisha viwanja mbalimba vya michezo kunaifanya Halmashauri ya wilaya ya Chunya kuwa Halmashauri ya kwanza ndani ya Mkoa wa Mbeya kumiliki uwanja, Jambo ambalo litapelekea Halmashauri ya wilaya ya Chunya kukusanya fedha nyingi pindi uwanja huo utakapokamilika na kuanza kutumika kwa mashindano na michezo mbalimbali

Gharama za ujenzi wa uwanja huo kutoka kwa Halmashauri ya wilaya ya Chunya Mpaka sasa shilingi milioni 104,160,800/= zimetumika kutoka Halmashauri ya wilaya ya Chunya huku gharama nyingine za ujenzi ambazo zinakadiliwa kufikia milioni 925,045,226.42/= (Fursa 667,272,500 na Fedha Tasilimu ni shilingi 257,772,726.42/=) zikiwa zimetumika awali wakati uwanja huo ukijengwa kwa michango na fedha za wadau kabla ya kuukabidhi kwa Halmashauri ya wilaya ya Chunya. Kwa Bajeti ijayo fedha Zaidi ya milioni 100 zimetengwa kuendeleza ujenzi wa uwanja huo

Kukamilika kwa uwanja huo itaongeza fursa kwa vijana wanamichezo kupata ajira kupitia michezo, wanachunya watapata eneo la kwenda kupata burudani lakini hamasa ya kufanya mazoezi kwaajili ya kulinda afya za wananchunya itaongezeka maana eneo la kufanyia mazoezi litakuwepo na hata watumishi mbalimbali watajipatia ajira kama vile walinzi, wahudumu na watu wengine wengi watapata ajira kwasababu ya uwepo wa uwanja huo.



Kituo cha Afya Sangambi kilichojengwa kwa Gharama ya shilingi milioni 463,000,000/= pia ni zao la fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ambapo sasa wananchi wa kata ya Sangambi yenye jumla ya watu 22,789 kwa mujibu wa sense ya watu na makazi ya mwaka 2022 wameondokana na adha ya kusafiri umbali mrefu kupata huduma mbalimbali za Afya hivyo kuendela kutumia muda mwingi kufanya shughuli za Maendeleo, hivyo uchumi wao kuimarika na baadaye uchumia wa Taifa kwa ujumla pia utaimarika Ujenzi wa Kituo cha Afya Sangambi na vituo vingine vinavyojengwa ndani ya wilaya ya Chunya unaenda sambamba na upatikanaji wa vifaa tiba ambapo kwa vituo vya Afya katika maeneo mbalimba vimeendelea kupata vifaa Tiba ambapo Kituo cha Afya cha Sangambi kimeshapata vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 50 na serikali inaendelea kukamilisha upatikanaji wa vifaa ili huduma zote zipatikane katika kituo hicho

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mpango kazi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya ni kuendelea kujenga miundombinu mbalimbali yenye lengo kumrahisishia mwananchi wa kawaida wa chunya kupata huduma bora, hivyo vituo vya afya, miundombinu ya shule na miundombinu mingine itaendelea kujengwa ama kuboreshwa kwa makubaliano rasmi kati ya viongozi na wananchi wenyewe kwa kupitia vikao mbalimbali vya maamuzi





# HABARI PICHA



*Timu ya wataalamu Kutoka Halmashauri ya wilaya ya Chunya, Bodi ya Tumbaku, Chama Kikuu cha Ushirika (CHUTCU), pamoja na Wadau kutoka katika makampuni ya Ununuzi wa Tumbaku wakiwa kwenye Tathimini ya zao la Tumbaku katika Mkoa wa kitumbaku Chunya.*

*Waheshimiwa Madiwani, wakuu wa Idara na vitengo, wageni waalikwa wakiwa kwenye Mkutano wa Baraza la madiwani, uliofanyika katika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.*



**OFISI YA MKUU WA MKOA MBEYA**

**MWENENDO WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI ZA MKOA WA MBEYA KUANZIA TAREHE 01 JULAI 2023 HADI TAREHE 02 FEBRUARI, 2024**

| Nafasi | Halmashauri | Makadirio ya Mwaka 2023/2024 | Hali ya Mapato ya ndani kufikia tarehe 02 Februari, 2024 | Asilimia iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Chunya DC | 5,543,358,000.00 | 7,195,655,850.03 | 130% |
| 2 | Rungwe DC | 6,179,615,000.00 | 5,172,878,468.65 | 84% |
| 3 | Busokelo DC | 2,000,000,000.00 | 1,620,848,981.76 | 81% |
| 4 | Mbarali DC | 6,750,801,000.00 | 5,207,597,690.29 | 77% |
| 5 | Kyela DC | 4,849,406,000.00 | 3,420,175,003.84 | 71% |
| 6 | Mbeya CC | 19,484,800,000.00 | 12,960,415,529.31 | 67% |
| 7 | Mbeya DC | 4,978,660,000.00 | 3,319,677,921.61 | 67% |
| **JUMLA KIMKOA** | | **49,786,640,000.00** | **38,897,249,445.49** | **78%** |

Chanzo: Halmashauri za Wilaya na Jiji Februari 02, 2024

*Halmashauri ya wilaya ya Chunya imeendelea kuziongoza Halmashauri za mkoa wa Mbeya katika Ukusanyaji wa mapato , kwa mujibu wa takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.*



***Baadhi ya Wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Kambikatoto Halmashauri ya wilaya ya Chunya wakipata Chakula Cha mchana Shuleni***




***Halmashauri ya wilaya ya Chunya imetoa chanjo ya Surua Rubella kwa watoto 44,942 sawa na asilimia 116.37 wakati lengo lilikuwa kuwafikia watoto 38,619 zoezi hili limefanyika kuanzia tarehe 15-02-2024 hadi tarehe 18-02-2024.***

# CHUNYA
## JARIDA LA MTANDAONI




## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

S.L.P 73 CHUNYA, MBEYA
SIMU: 025 2520121

www.chunyadc.go.tz
chunyadc_official
@ chunya_official
ded@chunyadc.go.tz

*Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*